**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI MILUNDIKWA**

**S.L.P 634,**

**SUMBAWANGA.**

**TAREHE 11/12/2020**

**Jina la Mwanafunzi...........................................................................**
**KIJIJI.........................................................................**

## MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MILUNDIKWA

### 1.0UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021.**Shule ya sekondari Milundikwa iko katika kijiji cha Kasu ,kata ya Nkandasi,wilaya ya Nkasi,Mkoa wa Rukwa.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**,unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** hivyo baada ya siku saba(7) unatakiwa uwe umeripoti shuleni vinginevyo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine.

### 2.0MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

**A.SARE YA SHULE**

**i/WAVULANA**

•**Suruali**:Anatakiwa awe na suruali mbili Darkbluu na Kaki.Mshono wa suruali;iwe na mifuko mitatu ,miwili mbele na mmoja nyuma upande wa kulia,miwili ya mbele iwe pande zote kulia na kushoto na sio kubandika,iwe na rinda mbili kila upande na upindo wa chini(miguuni) igeuzwe juu(turn up).Upana miguuni uwe wa kutosha isiwe ya kubana.Suruali za Mitumba na jinsi haziruhusiwi hapa shuleni.

•**Shati;**Awe na mashati mawili meupe(white) yenye mikono mifupi(short sleeve).

•**Viatu;**Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba,visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka pamoja na soksi rangi nyeupe.

•**Sweta**;Awe na sweta rangi ya Bluu yenye shingo (V) kwa ajili ya kujikinga na baridi.

•**Sare za Michezo;**Awe na Physical Training Short(P.T. Short) au Tracksuit rangi ya Blue na Raba za michezo.

•**Nywele**;Nywele ziwe fupi muda wote.

**ii/WASICHANA.**

Scanned with CamScanner

**•Sketi;**Anatakiwa awe na sketi mbili(2) Darkblue na Khaki,mshono wa sketi ziwe na rindabox kubwa nyuma na mbele.**NB:** Sketi ziwe ndefu,zifike kwenye viatu,sketi fupi hazitakiwi kabisa shuleni.Hivyo mzazi unatakiwa kumshonea binti yako sketi ndefu ili kuepuka usumbufu utakaojitokeza.

**•Shati**;Awe na mashati mawili meupe(white) yenye mikono mifupi(short sleeves).

**•Viatu;**Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba,visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka mbele na soksi nyeupe.

**•Sweta;**Awe na sweta rangi ya Bluu lenye shingo ya (V) kwa ajili ya kujikinga na baridi.

**•Sare ya Michezo;**Awe na Trucksuit rangi ya Bluu na raba kwa ajili ya Michezo.

**•Nywele;**Nywele ziwe fupi muda wote au ziwe zimesukwa vizuri mtindo wa roda (ziwe zimesukwa kurudi nyuma).

**B.VIFAA VYA MASOMO**

1.Daftari kubwa zisizopungua 12(CounterBook)
2.Mathematical set(MKEBE) 1.
3.Aje na kamusi moja ya kiingereza (Dictionary) moja.
4.Aje na kalamu za kutosha,rula na penseli.
5.Aje na cheti cha kuzaliwa(birth certificate).

## 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Kama ilivyo hata katika shule nyingine, Shule yetu pia inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria **Na.10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini.

***A: Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni:-***

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

Scanned with CamScanner

(i) Kutunza mali ya umma.

***B: Makosa yafuatayo yaweza kusababisha mwanafunzi kusimamishwa au kufukuzwa shule:-***

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
4. Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzako, mwalimu, mlezi na jamii nzima kwa ujumla.
5. Kupigana na mwanafunzi mwenzio, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
6. Kusuka mtindo usiotakiwa, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote wawapo shuleni.
7. Kufuga ndevu.
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
9. Uvutaji wa sigara .
10. Uasherati, mausiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa.
11. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
12. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi.
13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
16. Kudharau bendera ya Taifa.
17. Kufanya jaribio lolote lile la kujiua, au kutishia kujiua kama vile kunywa sumu n.k.
18. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB:Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU HII**

**……………**

**VINJE .I. MWASALA**

**(MKUU WA SHULE)**

**NAMBA YA SIMU:0765885667/0765663057**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MILUNDIKWA

Scanned with CamScanner

MILUNDIKWA SECONDARY SCHOOL,

P.O BOX 634,
SUMBAWANGA

MEDICAL OFFICER
…………………………………………..
…………………………………………..

RE:MEDICAL EXAMINATION

MR/MISS:…………………………………………………………………….

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for full time student in this school.The examination should include the following categories.

1.Hemoglobin……………………………………………………………………
2.P.VBleeding……………………………………………………………………
3.Sight……………………………………………………………………………
4.BloodPressure…………………………………………………………………
5.Urine for sugar and pregnancy…………………………………………………
6.Stool for routine examination…………………………………………………
7.Asthma…………………………………………………………………………
8.Skin diseases……………………………………………………………………
9.Leprosy…………………………………………………………………………
10.Pulmonary tuberculosis………………………………………………………
11.Nevereal diseases………………………………………………………………
12.Other serious diseases…………………………………………………………

MEDICAL CERTIFICATE

(To be compeleted by a Government Medical Officer)

1.I have examined the above named student and consider that He/She is physically fit/Unfit and mentally fit/Unfit for a full schooling.

2.Other comments………………………………………………………………

DATE……………………………………………………………………

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

NB:NENDA HOSPITALI NA FOMU KWA AJILI YA VIPIMO KISHA IRUDISHE SHULENI.

Scanned with CamScanner